SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

_____

(SURA YA 287)

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu** cha **153)

_____

SHERIA NDOGO (UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UTUNZAJI BORA WA ARDHI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO ZA MWAKA 2015

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Utangulizi na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo (Hifadhi ya Mazingira na Matumizi Bora ya Ardhi) za Halmashauri ya wilaya ya Kakonko za 2014 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Kakonko.

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakavyo fafanuliwa vinginevyo na Sheria yeyote andishi:-

"**Afisa Mtendaji**" maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kata au Afisa Mtendaji wa Kijiji husika;

"Afisa Mwidhinishwa" maana yake ni Afisa Maliasili, Afisa Kilimo na Mifugo, Mhandisi, Afisa Afya na mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"**Ardhi yenye madhara"** maana yake ni eneo la ardhi yoyote ambayo ikitumika inaweza kuhatarisha au kusababisha uharibifu wa mazingira katika ardhi hiyo au ardhi inayopakana nayo na ardhi ya aina hiyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa:-

.

(a) Ardhi iliyotengwa na Halmashuri kwa ajili ya kutupa taka.
(b) Ardhi iliyo kwenye miteremko na vilima vya Halmashuri.
(c) Ardhi au eneo lolote litakalobainishwa na kuidhinishwa na Halmashauri kutokana na umuhimu wake kimazingira,

"**Chanzo cha Maji**" maana yeke ni lambo la maji, kisima kilichoboreshwa au kuendelezwa na Halmashauri au kikundi cha watumiaji maji, kisima cha pampu ya maji kilichojengwa na Halmashauri au kinachomilikiwa na kikundi cha watumiaji maji kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"**Eneo la Hifadhi**" maana yake ni milima, maeneo ya vyanzo vya maji, misitu ya hifadhi ya Halmashauri, maeneo ya wazi (open spaces), vyanzo vya maji na eneo lolote litakalotengwa na kutangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya Hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya wilaya ya Kakonko;

"**Hifadhi ya mazingira"** maana yake ni utunzaji au hifadhi endelevu ya ardhi mimea, viumbe hai na visivyo hai, vyanzo vya maji na misitu ya hifadhi kwa kuzingatia masharti na maelekezo ya Afisa Muidhinishwa au Sheria Ndogo hizi;

"**Kilimo"** maana yake ni Kilimo cha mazao ya nafaka, ufugaji na miti kwa ajili ya chakula, biashara au misitu;

"Kijiji" au **"Kata**" maana yake ni Kijiji au Kata yoyote katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri;

"Kiwanda" maana yake ni eneo, jengo au kundi la majengo ambapo vitu vinatengenezwa kwa mikono au mashine na ni pamoja na gereji, karakana, vituo vya kuchomelea vyuma, kiwanda au mashine za kusindika au kukoboa nafaka, matunda au pamba;

"**Kuvuna misitu au mazao ya misitu**" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata, kung'oa miti, visiki, nyasi, magome ya miti, kuchimba mizizi ya miti, kupasua mbao au kuchuna kamba;

"**Maeneo yaliyotengwa**" maana yake ni maeneo yaliyotengwa na kutangazwa na Halmashauri ya Wilaya ua Halmashauri ya kijiji husika kuwa maeneo ya kilimo, ufugaji au malisho, misitu ya hifadhi, maeneo ya hifadhi , vyanzo ya maji au maeneo ya ardhi yenye madhara;

"Machinjio" maana yake ni machinjio ya Halmashauri au eneo lolote lililotengwa na kutangazwa na Halmashauri kuwa machinjio ya mifugo;

"**Mdau**" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha kijamii au asasi yoyote itakayo ruhusiwa na Halmashauri kujishughulisha na shughuli za kusafisha na kutunza mazingira katika eneo la Mamlaka ya wilaya;

"**Maji"** maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ni pamoja na maji ya kunywa , maji ya mito, vijito, maji yanayotiririka, maji yaliyohifadhiwa, maji yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maji yaliyo chini ya ardhi na maji yaliyo katika mkondo au chemi chemi;

Sura ya 191

"**Maji taka"** maana yake ni kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 ni pamoja na taka zitokanazo na kinyesi au zinazotirirka zikiwa na kinyesi, mkojo, uchafu wa maji maji kutoka katika majumba ya makazi, taasisi, majengo ya biashara na viwanda;

"**Mazao ya misitu**" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu, Sura ya 323, pamoja na miti,mazao yanayoota au kupatikana misituni,mianzi, magamba, mkaa, kuni, fito, mbegu za miti, nta, asali, matunda pori, majani, mizizi, magome ya miti, gundi au utomvu wa miti, matete, kamba, makuti, nyuzi za wanyama; pamoja na kitu chochote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa ni zao la misitu;

Sura ya 323.

"**Mazingira"** maana yake ni kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ni pamoja na maumbile halisi yanayowazunguka binadamu hewa,ardhi, maji, tabia ya nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, viumbe, hali za kibaolojia za wanyama, mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi;

Sura ya 191

"**Mfugaji**" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika ene lolote la Mamlaka ya Halmashauri;

"**Mifugo**"maana yake ni mbuzi, kondoo, ng'ombe, nguruwe wafugwao, punda, Mbwa na paka;

"**Mhandisi''**maana yake ni Mhandisi wa Ujenzi au Mhandisi wa Maji;

"**Mkurugenzi**" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya au mtumishi yeyote atakayekuwa anatekeleza majukumu ya Mkurugenzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

Sura ya 288

"Taka za kiwandani" kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu

usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sura ya 191 sehemu ya IX;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za wilaya); **Sura ya 288**

"**Kikundi cha watumiaji maji**" maana yake ni kikundi cha watu, kaya, taasisi, Kampuni, kikundi cha kijamii au shirika ambacho:-

(a) kimeanzishwa na kusajiliwa na Halmashauri kama kikundi cha watumiaji maji na kinamiliki chanzo cha maji au

(b) kinashughulika na kutunza mazingira pamoja na usafi wa mazingira

"Uchafu hatari" kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya191, maana yake ni kitu kigumu, chenye maji-maji, gesi au taka zitokazo kiwandani au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemikali kwa binadamu au mazingira; **Sura ya 191**

"**Uchafuzi wa mazingira**" kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamiziwa Mazingira, Sura ya 191, maana yake ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo moja kwa moja, joto, kemikali, biologia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambao unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali ya hatari kwa afya ya jamii, usalama au ustawi, au harari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu, au kizuizi ambacho ni sehemu ya mambo yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi; **Sura ya 191**

"**Rejesta**" maana yake ni rejesta ya kijiji au Halmashauri ya wilaya itakayoanzishwa na kutunzwa na Afisa Mtendaji au Afisa Muidhiniwa kwa ajili ya kusajiri:-

(a) Vikundi vya watumiaji maji
(b) Wafugaji na wakulima katika eneo husika
(c) Vikundi vya utunzaji na usafi wa mazingira;

"Udongo" kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, Madini, uoto wa mimea, **Sura ya 191**

mimea na wanyama walio chini ya udongo pamoja na vumbi.

"**Vitu hatari"** kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, maana yake ni kemikali yoyote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea, wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira.

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana na Serikali za mitaa **Sura ya 288**

SEHEMU YA PILI

MASHARTI YA UFUGAJI NA HIFADHI YAMAZINGIRA

Wajibuwa mfugaji

4. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila mfugaji atatakiwa:-

(a) Kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoamriwa na Halmashauri;

(b) Kufuga na kulisha mifugo yake kama katika maeneo yaliyopangwa na Halmashauri;

(c) kupitisha mifugo yake katika njia (livestock routes) zilizopangwa na Halmashauri;

(d) Kuwa na Kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) Kupeleka mifugo katika josho kama itakavyoagizwa na Halmashauri;

(f) Kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

(g) Kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa ghararma itakayopendekezwa na Halmashauri;

(h) Kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;

(i) Kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;

(j) Kuhudhuria mafunzo ya ufungaji kama atakavyohitajiwa na Halmashauri

(k) Kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o.

(2) Bila kuathiri kifungu cha 4 (1) (a) na kifungu cha 7 cha sheria hii, ni marufuku kwa mtu yoyote kufuga mifugo katika eneo la mjini isipokuwa kwa mujibu wa sheria za mipango miji.

5. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Halmashauri itakuwa na wajibu na majukumu yafuatayo:-

(a) Kusaidia na kuelekeza Halmashauri za vijiji kutenga ardhi na kupanga matumizi bora ya ardhi kulingana na mahitaji na ukubwa wa ardhi katika kijiji husika.
(b) Kutenga na kuandaa njia za kupitisha mifugo kwenda na kutoka malishoni, minadani, sokoni au gulioni katika eneo la Halmashuri.
(c) Kusimamia na kuratibu shughuli za kilimo,ufugaji na maendeleo ya mifugo
(d) Kuhakikisha kuwa kila Mtaa, Kata na Halmashauri ya kijiji inaanzisha na kutunza rejesta ya wakulima na wafugaji.
(e) kufanya sensa kwa ajili ya kuhesabu na kuratibu idadi ya mifugo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri.

6. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote yule:- **Mambo yasiyoruhusiwa.**

(a) Kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo au vyanzo vya maji ambavyo havikutengwa kwa ajili hiyo;
(b) Kusafirisha, kupitisha au kuswaga mifugo kwa kuipitisha barabarani
(c) Kuwa na kibali cha kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri ambacho hakikutolewa na Afisa Mwidhinishwa.
(d) Kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;
(e) Kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo minada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri.
(f) Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri;
(g) Kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kupitisha mifugo.

7. — (1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashari ambapo hapakutengwa au kuruhusiwa kuchungia mifugo.

Kudhibiti mifugo inayozurura hovyo

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama itakavyopangwa na Halmashauri na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

(3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya

muda wa siku saba (07) tangu kukamatwa kwa mifugo Mkurugenzi atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mifugo au baada ya kuomba na kupata idhini ya Mahakama ya Wilaya.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi kutoka katika fedha za mauzo ya mifugo kwa mnada na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika hazina ya Halmashauri na kukatiwa stakabadhi.

(5) Endapo mwenye mifugo au mfugo huo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake ndani ya muda wa siku 14 Halmashauri itarudisha fedha zake.

(6) Endapo itatokea kufa kwa mfugo au mifugo yoyote Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote.

8.— (1) Itakuwa Halali kwa Afisa Kilimo na Mifugo, maafisa watendaji wa Kata na Vijiji, na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au jengo lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

Ukaguzi wa Mifugo.

(2) Mtu yeyote atakaye mzuia Afisa yeyote Mwidhinishwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya Tshs 50,000/= au kufungwa jela kwa kipindi cha miezi sita.

(4) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

(5) Kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhinishwa atakuwa na majukumu na wajibu ufuatao:-

Wajibu wa Afisa Mwidhinishwa.

(a) Kuingia katika nyumba, zizi la mifugo au jengo lolote kati ya saa 1.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni kwa ajili ya kukagua, kuhesabu mifugo na kutoa ushauri.
(b) Kuchukua hatua za Kisheria katika Mahakama dhidi ya mfugaji yeyote aliyekiuka Sheria Ndogo hizi na kukusanya faini itakayoamriwa na Mahakama kwa kuzingatia taratibu za kukusanya mapato ya Halmashauri.
(c) Kutoa taarifa kwa Halmashauri na Mkurugenzi endapo mifugo itakuwa imekamatwa na hatua za Kisheria zinatakiwa kuchukuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.
(d) Kuhakikisha kwamba Halmashauri za Vijiji katika kila Kata zina maeneo yaliyotengwa
(e) Kuhakikisha kwamba Sheria Ndogo hizi zinatekelezwa
(f) Kuhakikisha kwamba mifugo inasafirishwa au kuingizwa katika eneo la Halmashuri baada ya kupata kibali
(g) Kuhakikisha kwamba mifugo yote inachinjwa katika machinjio ya Halmashauri au maeneo yaliyoidhinishwa kuwa machinjio.
(h) Kuhakikisha kuwa mifugo inapelekwa katika Vituo vya chanjo au majosho kwa ajili ya matibabu.

9. — (1) Wafugaji wote wanatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 9 (4) cha Sheria ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Taratibu za ufugaji, uuzaji na uchinjaji wa mifugo

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni kwa ajili ya kuchinja mfugo au mifugo mahali ambapo pametengwa na Halmashauri kama machinjio.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi mtu yeyote ambaye ni mfugaji, mmiliki, muuzaji, mchinjaji au mnunuzi wa mifugo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri:-

(a) Endapo atataka kuchinja mfugo au mifugo atachinja mfugo au mifugo hiyo katika machinjio au mahali popote ambapo palipoidhinishwa na Halmashauri kuwa machinjio.

(b) Endapo atakuwa anasafirisha, kupitisha au kuingiza mifugo ataomba na kupata kibali cha Halmashauri.

(c) Atapeleka mifugo yake kwenye majosho au Vituo vya tiba vilivyoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kupata tiba.

(d) Atatoa taarifa kwa Afisa muidhinishwa endapo kutatokea mlipuko wa magonjwa ya mifugo.

(e) Atauza, kununua au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika mnada, gulio au soko lililoidhinishwa na Halmashauri.

SEHEMU YA TATU

KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

Taratibu za Kilimo
Sura ya 113; Sura ya 114 na Sura ya 191.

10.—(1) Mtu yeyote atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia masharti na taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi au Sheria zilizotungwa na Bunge.

(2) Kwa aijli ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi itakuwa halali kwa Afisa Kilimo kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi.

11.—(1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ni marufuku kwa mtu yeyote:-

(a) Kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kando kando ya mito, bwawa, au kufanya

jambo au shughuli yoyote itayoharibu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo.

(b) Kutumia ardhi yoyote katika eneo la Halmashauri kinyume na matumizi yaliyotengwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(c) Kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa kutumia moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashauri.

(2) Kibali kitakachotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye shamba, tarehe, eneo analotaka kuchoma moto**.**

(3) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi muda unaotakiwa kuchoma moto ni kuanzia majira ya saa 12:00 asubuhi hadi saa 5:00 asubuhi na mtu yeyote atakayechoma moto nje ya muda huu ulioainishwa katika kifungu cha 13 (3) cha Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini ya shilingi 50, 000/= au kutumikia kifungo cha miezi kumi na mbili jela.

(4) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa inazuia kilimo cha kuhama hama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

Uhifadhi waUoto wa asili.

12. Ni wajibu wa kila mkazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanarudisha eneo hilo katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto kurudi katika hali yake.

Uchimbaji wa mchanga na kokoto.

13. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ni marufuku kwa mtu yeyote:-

(a) Kuchimba mchanga, mawe, kokoto au kufanya shughuli za kufyatua matofali katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi, maeneo yaliyohifadhiwa, kando kando ya vyanzo vya maji au bwawa isipokuwa kwa ruhusa maalum ya Halmashauri.

(b) Kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi

SEHEMU YA NNE

HIFADHI YA MISITU

Ukataji miti katika Maeneo yaliyohifadhiwa

14. — (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, ni marufuku kwa taasisi au mtu yeyote:-

(a) Kuchoma moto misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko katika eneo la Halmashauri.
(b) Kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.
(c) Kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.
(d) Kuchoma mkaa katika eneo lililohifadhiwa au eneo lolote bila kibali cha Halmashauri.

(2) Iwapo utatokea moto katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya Hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na mdahara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katka eneo hilo.

Kuchoma na kusababisha moto; kibali cha kuchoma moto.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, na kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

(4) Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto.

(5) Halmashuri itatakiwa kuhakiki kama miti iliyovunwa imekomaa na inafaa kw ajili ya matumizi

Wajibu wa kupanda miti

15. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ni wajibu wa kila taasisi na mkazi yeyote katika eneo la Mamlaka ya Halmashuri:-

(a) Kupanda na kutunza miti katika eneo lake
(b) Kupanda na kutunza miti katika maeneo yake
(c) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki

16. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri kitakuwa na wajibu wa:-

(a) Kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili kwa matumizi ya baadaye;
(b) kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji;
(c) Kuhakikisha kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi (10) kwenye eneo la nyumba yake;
(d) Kuhakikisha kwamba mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti wa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo ana kibali kilicho tolewa na Afisa Misitu kwa misitu iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri.
(e) Kutenga, kupanda na kutunza shamba la miti ekari zisizopungua mbili.
(f) Kuhakikisha kwamba taasisi zote za shule zilizoko katika eneo la kijiji zimepanda miti katika maeneo ya taasisi hizo kwa ajili ya kukinga upepo na hifadhi ya mazingira.
(g) Kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye vilima,makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;
(h) Kuhakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga ya upepo.
(i) Kuhakikisha kwamba kila mtu mwenye nyumba kwenye eneo la mpango miji au mji mdogo anapanda miti kando kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake kwa kuzingatia maelekezoyaMwidhiniwa.

SEHEMU YA TANO

HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

17.— (1) Itakuwa ni jukumu na wajibu wa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi:- **Wajibu na jukumu la Halmashauri kulinda vyanzo vya maji**

(a) Kuanzisha, kusimamia, kulinda, kuratibu vyanzo vyote vya maji na vikundi vya watumiaji maji vilivyo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri
(b) Kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakaye haribu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

(2) Bila kuathiri kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, taasisi, kampuni, mmiliki yeyote wa kiwanda, shirika au mtu binafsi anaweza kuomba kwa Halmashauri kibali cha kuanzisha na kumiliki eneo kwa ajili ya kutupa au kuchoma taka zinazozalishwa katika eneo analomiliki.

18.—(1) Ni marufuku kwa taasisi au mtu yeyote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira. **Kulinda eneo la Hifadhi**

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri:-

(a) Kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.
(b) Kushirikana na vikundi vya kijamii katika eneo la Mamlaka ya Halmashuri kupanda miti na kutunza maeneo yaliyohifadhiwa**.**

(3) Ni marufuku kwa taasisi au mtu yeyote kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi:-

(a) Kumilki eneo la chanzo cha maji isipokuwa Halmshauri.

(b) Kujenga kwa kuelekeza mabomba ya maji safi au taka kwenye mifereji au mitaro ya barabara, bwawa, visima au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, wanyama au viumbe hai.
(c) Kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

SEHEMU YA SITA

TAKA NGUMU NA LAINI

Utupaji wa taka ngumu na laini

19.— (1) Ni jukumu na wajibu wa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutenga eneo au maeneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi wa eneo la Mamlaka ya Halmashauri.

(2) Mtu yeyote atakayetupa hovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia katika kingo za mifereji ya barabara, maeneo ya barabara, bwawa, au kwenye vyanzo vya maji vilivyo katika eneo la Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri katika kudhibiti taka

20. Katika kuhakikisha kwa umma unashirikishwa katika shughuli za udhibiti wa taka ngumu, laini na usafi wa Mji kwa ujumla Halmashauri itakuwa na wajibu wa:-

(a) Kuhamasisha uundaji wa vikundi jammii (CBOs) katika kila Kata za Mjini na kuzishirikisha katika shughuli za udhibiti wa taka ngumu na laini katika maeneo ya Kata husika.
(b) Kuingia mkataba na kikundi jamii (CBO) au wakala yeyote kwa ajili ya kukusanya na kuzoa taka ngumu na laini kwa ajili ya usafi wa mazingira, na kuzipa nguvu za Kisheria katika kutetea maslahi zake zitokanazo na mikataba ya usafi wa mazingira na uzoaji taka kati ya CBOs na Halmashauri.
(c) Kuratibu kusimamia mtu au mkazi, kiwanda, taasisi au kampuni zenye umiliki wa maeneo ya kutupa, kuchoma au kutiririsha taka zozote na shughuli za kuzoa taka na kusafisha mazingira.
(d) Kusajili wadau au kikundi chochote cha jamii kinachojishughulisha na uzoaji wa taka au wakazi wa kitongoji chochote katika Halmashauri kuhusu usafi na mkakati wa kufanya usafi wa mazingira katika eneo lolote Halmashauri.
(e) Kuelekeza kaya au wakazi mahali panapostahili kutupa au kuchoma taka.
(f) Kuweka na kuidhinisha kiwango cha tozo, taasisi, kampuni, kiwanda au mkazi yeyote kama mchango wa kuchangia shughuli za uzoaji taka na usafi wa mazingira.

21. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine za kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matuda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu, vituo au stendi za mabasi ya abiria au kushushia mizigo bila kuzingatia taratibu za ujenzi.

Uendeshaji wa viwanda

SEHEMU YA SABA

MAKOSA NA ADHABU.

22. Bila kuathiri masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi mtu yeyete atakuwa ametenda kosa ikiwa:-

(a) Atatutupa hovyo taka za aina yeyote, kujisaidia haja ndogo au kubwa katika au karibu na chanzo cha maji, kuanzisha dampo la taka au karibu na makazi ya watu.
(b) Ataendesha shughuli za karakana, kiwanda mashine ya kusaga au kuranda mbao, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu hatari kwa binadamu au viumbe hai katika maeneo ya makazi, soko, stendi au kituo cha mabasi, au maeneo yaliyohifadhiwa.
(c) Ataanzisha kiwanda au taasisi au chochote katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa ajili ya taasisi au viwanda.
(d) Atajenga nyumba za makazi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuwa wazi(open space) viwanda hifadhi ya mazingira au chanzo cha maji
(e) Atafulia nguo, kuosha vyombo au magari, kuoga , kutupa taka zozote karibu na vyanzo vya maji au eneo ambalo halikutengwa kwa Ajili hiyo.

23. Mtu au mkazi yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa:-

Makosa yanayohusu mifugo na ufugaji

(a) Ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali
(b) Atasafirisha au kutoa mifugo bila kuwa na kibali

(c) Atalisha mifugo katika maeneo ambayo hayaruhusiwi.
(d) Atafuga mifugo zaidi ya idadi inayoruhusiwa

(e) Hataandikisha au kutoa taarifa ya idadi ya mifugo aliyonayo kwa Afisa Mwidhinishwa

Makosa yanayohusu kilimo na hifadhi ardhi

24. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kuchoma moto, maeneo ya kilimo bila kibali, kukiuka masgggharti ya kuhifadhi ardhi, kulisha mifugo katika maeneo ya kilimo, kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya mifugo au misitu ya hifadhi atakuwa ametenda kosa

Makosa yanayohusu vyanzo ya maji

25. Mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji atakaye shindwa kuhifadhi vyanzo vya maji na viumbe wengine, atakuwa ametenda kosa.

26. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo mtu yeyote atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiani atalipa faini ya shilingi 50, 000/= kwa kosa lolote atakalotenda kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 26 (a) hadi (l) cha Sheria Ndogo hizi:-

(a) Atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali cha Afisa Mwidhinishwa
(b) Atashindwa kushiriki katika kuzima moto, au
(c) Atavuna mazao ya misitu katika misitu au maeneo yaliyohifadhiwa au yasiyohifadhiwa bila kibali au misitu bila kibali au.
(d) Atachoma mkaa au atakata kuni bila kibali, au
(e) Atachoma au kusababisha moto misitu bila kujali, au
(f) Atavuna mazao ya misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali, au
(g) Atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali au kuvuna mazao ya misitu, au
(h) Atafyeka nyasi, kuong'oa vichaka na kuong'oa visiki kwenye misitu bila kibali.
(i) Atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au iliyohifadhiwa kama bustani ya miti.
(j) Atakata miti au kuingiza mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kikinga upepo.

(k) Atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mazingira na vitu vingine bila kuwa na kibali.

(l) Atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zilizohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngum na laini

27. Mtu yeyote atakayetupa hovyo taka ngumu au taka laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa na Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa ametenda kosa.

28. Mtu yeyote atakayetiririsha hovyo maji machafu, sumu, kemikali au taka zozote laini atakuwa ametenda kosa la uchafuzi wa mazingira.

Makosa yanayohusu viwanda

29. Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiwanda, viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga au kukoboa nafaka, mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu au kinyume cha Sheria ya Mpango Mji na VIjiji atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu Kilimo

30. Mtu yeyote atakaye endesha shughuli za ufugaji au kilimo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa ajili ya shughuli hizo atakuwa ametenda kosa.

Adhabu.

31. Bila kuathiri kifungu cha 26 cha Sheria Ndogo hizi mtu yeyote atakayevunja au kukiuka Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (Tshs 300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani kifungo na faini.

Lakiri ya Halmashauri ya wilaya ya Kakonko imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kutokana na Azimio la Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika vilivyo tarehe……..Mwezi……Mwaka…… mbele ya:-